# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 25 APRIL 2025

Kwa wiki inayoishia tarehe 25 April 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yalipungua kwa asilimia 49.03 kutoka TZS 7 bilioni hadi TZS 3.57 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua pia kwa asilimia 76.23 kutoka hisa milioni 18.75 hadi hisa milioni 4.46.

Jumla ya Mtaji wa Soko uliongezeka kwa asilimia 0.10 kutoka TZS 18.9 trilioni hadi TZS trilioni 18.92.

Hii nikutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za JHL,AFRIPRISE,MBP na KCB,ambapo JHL iliongezeka bei kwa asilimia 0.49 , AFRIPRISE ikiongezeka bei kwa asilimia 4.26,MBP ikiongezeka bei kwa asilimia 2.6 na KCB ikiongezeka bei kwa asilimia 1.27.

Mtaji wa Soko la Ndani ulipungua kwa asilimia 0.08, kutoka TZS 12.984 trilioni hadi TZS 12.97 trilioni kutokana na kupungua kwa bei ya hisa za TPCC ambazo zilipungua kwa TZS 40, TCCL ambazo zilipungua kwa TZS 40, MKCB ambazo zilipungua kwa TZS 30 na NICOL ambazo zilipungua kwa TZS 30.

CRDB iliongoza kwa idadi kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 95.81 sawa na hisa milioni 4.2. ikifuatiwa na AFRIPRISE kwa asilimia 1.2 sawa na hisa 53,360 .

CRDB imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 3.3 bilioni, ambayo ni 94.46% ya mauzo yote ikifuatiwa na TPCC Ikirekodi TZS 60million ambayo ni asilimia 1.69%, huku NMB ikirekodi 58 million ambayo ni sawa na asilimia 1.64% ya mauzo yote.

Wawekezaji wa ndani wamechangia asilimia 99.95 huku wawekezaji wa kigeni wakichangia asilimia 0.05 tu kwenye shughuli za soko wiki hii.

Katika wiki kulikuwa na miamala 88 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 11.98 bilioni.

Mnada wa dhamana za Serikali za muda mfupi (Treasuty bill ) wa siku 35,91,182,364 uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 23 April 2025, ulisajili zabuni 39 ambapo zabuni 22 zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 65.7Bilioni.